**SHERIA YA KAMISHENI YA WAKFU NA MALI YA AMANA**
**NAM.2 YA MWAKA 2007**

# KANUNI ZA HIJJA, 2019

ZANZIBAR

JULAI, 2019

## SHERIA YA KAMISHENI YA WAKFU NA MALI YA AMANA NAM 2 YA MWAKA 2007

## KANUNI ZA HIJJA

**(Chini ya kifungu cha 67)**

KWA UWEZO niliopewa chni ya kifungu cha 67 cha Sheria ya Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana, Nam,2 ya mwaka 2007. Mimi Khamis Juma Maalim, Waziri wa Katiba na Sheria Zanzibar, natunga kanuni zifuatazo:

Jina fupi na kuanza kutumika

1. Kanuni hizi zitajulikana kuwa ni Kanuni za Hijja za mwaka, 2019 na zitaanza kutumika mara tu baada ya kusainiwa na Waziri na kutangazwa katika Gazeti.

Ufafanuzi

2. Katika Kanuni hizi isipokuwa maelezo yakihitaji vyenginevyo, maneno haya yametafsiriwa kama ifuatavyo:

"Biitha" maana yake ni Ofisi au Utaratibu wa kuendesha shughuli za Hija kama ulivyoanzishwa kwa mujibu wa Miongozo inayotolewa na Wizara ya Hijja ya Saudi Arabia ili kuratibu mawasiliano yanayohusiana na shughuli za Hijja baina ya Saudia na nchi nyenginezo.

"Bodi" maana yake ni Bodi ya Uongozi ya Kamisheni.

"Gazeti" maana yake ni Gazeti Rasmi la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

"Kamisheni" maana yake ni Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana.

"Kampuni" maana yake ni Taasisi iliyosajiliwa rasmi kuandaa safari za Hijja Zanzibar.

"Katibu Mtendaji" maana yake ni Katibu Mtendaji kama ilivyofafanuliwa chini ya kifungu cha 9 cha Sheria ya Kamisheni.

"Mnadhimu" maana yake ni Kiongozi wa Kampuni anayetambulishwa rasmi katika Mamlaka za Hijja nchini Saudi Arabia.

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana Namba 2 ya mwaka 2007 pamoja na marekebisho yake.

"Tirka" maana yake ni mali au haki ya kimali aliyoiwacha mtu baada ya kifo chake.

"Umoja" maana yake ni umoja rasmi unaotambuliwa na Kamisheni kuwakilisha Kampuni na Taasisi zote za Hijja.

"Waziri" maana yake ni Waziri anayesimamia Sheria ya Wakfu na Mali ya Amana.

Vibali vya kusafirisha mahujaji

3. Kutakua na aina mbili za vibali ya kusafirisha mahujaji ambavyo vitatolewa na Kamisheni

(1) Vibali vya kudumu ambavyo vitatumika kwa muda wa miaka mitano na zitapewa Kampuni zilizokidhi masharti na miongozo yote ikiwemo:

a. Kusafirisha mahujaji wasiopungua 50;

b. Kuwa na dhamana ya Benki yenye thamani kama itakavyobainishwa na Bodi baada ya kushauriana na Umoja.

c. Kuwa na viongozi wenye sifa zilizoainishwa katika para ya 9, 10 na 11 ya Kanuni hizi.

(2) Vibali vya muda ambavyo vitatumika kwa muda wa miaka mitatu na vitatolewa kwa Kampuni mpya au zilizowekwa katika uangalizi maalumu wa Kamisheni.

(3) Kampuni inaweza kuwekwa katika uangalizi maalumu wa Kamisheni, iwapo kibali chake cha kudumu kitafutwa; na Kamisheni ikaridhia kuwa iendelee kutoa huduma kwa makubaliano maalumu na Kamisheni

Utaratibu wa kuomba Kibali

4. Ili Kampuni ipatiwe kibali cha kusafirisha mahujaji na Kamisheni italazimika kukamilishe masharti yafuatayo:-

(1) Iwe imesajiliwa rasmi Zanzibar; au ipate kibali cha kufanya kazi zake Zanzibar kwa mujibu wa Sheria za Zanzibar.

(2) Ibainishe wazi katika Katiba au Hati yake kuwa miongoni mwa malengo yake ni kuandaa safari za Hijja.

(3) Iombe kwa maandishi kwa Katibu Mtendaji ridhaa ya kukasimiwa jukumu au kuwa wakala wa kuanda safari za Hijja. Ombi hilo liambatanishwe na: a- Hati ya usajili wa Kampuni. b- Majina na sifa za Mnadhimu, Sheikh na Daktari wa Kampuni.

c- Dhamana ya Benki (*bank guarantee*) ya asilimia kumi (10%) ya gharama kulingana na idadi ya mahujaji itakayoomba kusafir

d- Kufuata maelekezo au kuwasilisha vielelezo vya ziada vitakavyotakiwa na Katibu Mtendaji baada ya kufanya uhakiki na kabla ya kutoa uamuzi.

e- Kampuni iliyokataliwa kupata kibali inaweza kukata rufaa kwa Waziri ndani ya siku 30 za kalenda baada ya kupata barua ya kukataliwa.

(4) Kampuni zote ambazo kabla ya kuanza kutumika kwa Kanuni hizi zilikuwa zikisafirisha mahujaji kwa idhini ya Kamisheni, zitapatiwa kibali cha kudumu

Kumalizika kwa matumizi ya Kibali

5. Kibali cha kusafirisha mahujaji kitasita kutumika iwapo:-

(1) Muda wake wa matumizi umemalizika.

(2) Kampuni imefutiwa usajili au kusimamishwa na Mrajisi wa Makampuni.

(3) Kampuni imefutwa au kusitishwa rasmi kutoa huduma za Hijja nchini Saudi Arabia na vyombo vyenye dhamana ya Hijja nchini humo.

(4) Kitafutwa na Kamisheni baada ya Kampuni kupoteza sifa za kupatiwa kibali au sifa za Kampuni zinazosafirisha mahujaji.

(5) Kampuni itashindwa kusafirisha mahujaji kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo.

(6) Kampuni itashindwa kufikisha idadi ya chini iliyowekwa ya Mahujaji kwa kipindi chamiaka mitatu mfululizo.

6. Bila ya kuathiri kifungu cha 5 cha Kanuni hizi, Kamisheni itaipatia Kampuni barua ya indhari ya kumalizika matumizi ya kibali na kuiarifu sababu.

(1) Kampuni itapewa muda wa siku 30 za kalenda ili kujitetea iwapo haikuridhika na sababu za kusitishwa matumizi ya Kibali chake.

(2) Iwapo Kampuni haikuridhia maamuzi ya kufutiwa Kibali na Kamisheni inaweza kukata Rufaa kwa Waziri.

Kampuni iliyofutiwa Kibali

7. (1)Kamisheni kwa kushauriana na Biitha na Umoja wataweka utaratibu utakaohakikisha kuwa haki na wajibu wa Kampuni iliyofutiwa kibali zinasimamiwa kwa uadilifu.

(2) Kamisheni inaweza kuipatia Kibali cha Muda Kampuni iliyositishwa kwa kuiweka chini ya uangalizi maalumu kama itakavyoona inafaa.

(3) Viongozi wa Kampuni zilizofutiwa kibali hawatoruhusiwa kuunda Kampuni nyengine ndani ya kipindi cha miaka mitatu.

Sifa za Kampuni zinazosafirisha Mahujaji

8. Kampuni itakayopata kibali cha kusafirisha mahujaji italazimika :-

(1) Kufuata miongozo, taratibu na sharti zinazowekwa na Kamisheni na Biitha.

(2) a- Kuwa mwanachama wa kudumu au wa muda katika Umoja; au b - Kupata usajili wa kupeleka mahujaji kama Shirika linalojitegemea katika Mamlaka husika za Saudi Arabia.

(3) Kushikamana na adabu za Kiislamu na miamala inayozingatia Shariah.

(4) Kutoa mashirikiano na msaada kwa Kampuni nyenginezo.

(5) Kutoa kila aina ya msaada kwa mahujaji kila inapolazimu bila ya kujali Kampuni au jinsia au uraia wake.

(6) Kushikamana na miamala inayozingatia maadili mema na sharia za nchi.

(7) Kutoa taarifa kwa wakati kila inapohitajika na Kamisheni, Biitha na Umoja.

(8) Kampuni itakayosafirisha mahujaji 100 na ziada ni lazima iwe na madaktari wawili mmoja wao akiwa ni mwanamke.

9. Ili mtu akubalike kuwa Mnadhimu wa Kampuni ni lazima awe na sifa zifuatazo:-

a) Awe ni raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Sifa za Mnadhimu

b) Awe na umri usiopungua miaka 25 na usiozidi miaka 65.

c) Awe na afya njema na uwezo wa kufanya kazi katika mazingira magumu.

d) Aweze kusoma, kuandika na kuzungumza lugha ya Kiarabu au Kiingereza.

e) Awe na tabia njema, subra, hekma na mlahaka mzuri.

f) Awe hajawahi kutiwa hatiani kwa kosa la jinai au utapeli ndani kipindi cha miaka 10.

g) Awe ameshatekeleza Ibada ya Hijja na mwenye uzowefu wa kutosha katika kazi ya kuhudumia mahujaji kama kiongozi kwa muda usiopungua miaka mitatu.

Sifa za Sheikh

10. Ili mtu afae kuwa ni Sheikh wa Kampuni ni lazima awe na sifa zifuatazo:-

a) Awe na umri usiopungua miaka 25 na usiozidi miaka 70.

b) Awe na elimu ya Dini ya Kiislamu isiyopungua Diploma au inayofanana na kiwango hicho.

c) Aweze kuzungumza lugha ya Kiswahili na Kiarabu.

d) Awe na utaalamu wa Fiqhi ya Hijja na uwezo wa kuwafikishia mahujaji.

e) Awe ameshawahi kutekeleza Ibada ya Hijja na kufanya shughuli ya kiuongozi katika Hijja.

f) Awe muaminifu, mwenye tabia nzuri, subra, hekma na mlahaka mzuri.

g) Awe na afya njema.

Sifa za Daktari

11. Ili mtu afae kuwa ni daktari wa Kampuni ni lazima awe na sifa zifuatazo:-

a) Awe Muislamu na mwenye tabia, njema subra, hekma na uwezo wa kufanya kazi katika mazingira magumu.

b) Awe anatambuliwa na amesajiliwa na Bodi ya Madaktari.

c) Awe anafahamu lugha ya Kiswahili na Kiingereza au Kiarabu.

d) Awe na uzowefu wa kazi ya udaktari kwa muda usiopungua miaka mitatu.

e) Awe tayari kufuata miongozo na taratibu zinazotolewa na Biitha na Wizara zinazohusiana na mambo ya Afya kwa Tanzania.

Haki na Wajibu wa Kampuni

12. Kampuni itakuwa na haki ya kupatiwa fursa, taarifa, huduma na kila aina ya msaada unaopatiwa Kampuni zinazosafirisha mahujaji Zanzibar, ili ziweze kutoa huduma zinazostahiki kwa usahihi, wepesi na ubora wa hali ya juu.

(1) Kampuni italazimika kusifika na Sifa za Kampuni Zinazosafirisha Mahujaji Zanzibar kama zilivyobaonishwa katika Kanuni ya 8.

(2) Kampuni italazimika kutoa taarifa, vielelezo, michango na ada zilizowekwa na Kamisheni, Biitha na Umoja kwa wakati, usahihi na ukamilifu.

(3) Kampuni italazimika kuandaa kwa maandishi na kumpatia kila hujaji, Kamisheni, Biitha na Umoja kipeperushi kinachoelezea kwa muhtasari huduma atakazopewa hujaji ambacho kitazingatiwa kuwa ndio mkataba wake wa huduma.

13. (1)Kutakuwa na Umoja wa Taasisi za Hijja Zanzibar, uliosajiliwa rasmi na Mrajisi wa Makampuni na kufanya kazi zake kwa mujibu wa *Memorandam* ya kuanzishwa kwake.

Haki na Wajibu wa Umoja

(2). Umoja utakuwa na haki ya kupatiwa na Kamisheni fursa zote zinazopatiwa taasisi zenye hadhi kama ya Umoja huo hapa Zanzibar, na kila aina ya msaada utakaouwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

(3) Umoja utalazimika kufanya kazi zake kwa mujibu wa sheria na kanuni zilizopo Zanzibar;

(4) Umoja utalazimika kutoa mashirikiano ya hali ya juu kwa Kamisheni, Biitha na vyombo vyote vyenye uhusiano na Umoja kwa lengo la kuimarisha huduma za Hijja Zanzibar.

(5)Umoja utaandaa Ripoti ya Hijja ya mwaka ambayo itatoa takwimu za kina za kila Kampuni na kuiwasilisha kwa Katibu mtendaji si zaidi ya

mwezi 15 Safar ya kila mwaka wa Hijiria. Ripoti hiyo ijumuishe pia mambo yafuatayo:

a) Utangulizi.
b) Maadalizi ya Hijja kuanzia thathmini hadi safari.

c) Utekelezaji halisi kuanzia kufika Saudia hadi kufika nyumbani
d) Taarifa inayohusiana na Afya.
e) Hitimisho itakayotoa tathmini ya jumla, changamoto na mapendekezo.

Haki na Wajibu wa Mahujaji na Biitha

14. Kamisheni na Biitha zitakuwa na haki ya kupatiwa na Umoja pamoja na Taasisi taarifa, vielelezo, ada, michango, ushauri na ushirikiano wa hali ya juu ili zimudu kutoa huduma kwa uadilifu, wakati na ubora wa hali ya juu.

(1). Kamisheni na Biitha zitalazimika kutoa msaada, ushauri, ushirikiano, taarifa, miongozo na yale yanayohitajika katika kuimarisha huduma za Hijja kwa uadilifu na usawa kwa Umoja, Kampuni ya Hijja na Mahujaji.

(2). Kamisheni na Biitha zitawajibika kutekeleza majukumu yake ipasavyo kama yalivyoelezwa katika Sheria, Kanuni, Miongozo, mikataba na makubaliano yanayofikiwa nchini na nje ya nchi.

(3). Kamisheni na Biitha zitalazimika kutunza taarifa za siri za Umoja, Kampuni na Mahujaji kwa daraja ya usiri wake.

(4)Kamisheni na Biitha zitakuwa na wajibu wa kuushirikisha Umoja katika kujadili mambo ambayo yana maslahi ya Umoja na Kampuni.

15. Mahujaji watakuwa na haki kusikilizwa na Kamisheni, Biitha na Umoja; kuongozwa na kusaidiwa ili kupata haki wanayostahiki kutoka katika kampuni waliyojisajili.

Haki na Wajibu wa Mahujaji

(1) Mahujaji watakuwa na haki ya kupatiwa taaluma na huduma kwa mujibu wa mkataba wa huduma waliokubaliana na Kampuni.

(2) Mahujaji watakuwa na wajibu wa kulipia malipo yao katika muda uliowekwa, kutoa taarifa zinazotakiwa, kufanya uchunguzi wa afya, kutafuta hati za kusafiria na yale yote atakayotakiwa kuwasilisha katika Kampuni kwa mujibu wa mkataba na taratibu zilizopo.

(3) Mahujaji watakuwa na wajibu wa kutoa taarifa yoyote itakayohitajika

Kamisheni, Biitha au katika Umoja yenye lengo la kuleta ufanisi katika Hijja au kutatua jambo lolote lililotokea au kuwasilishwa katika vyombo hivyo au vyenginevyo vinavyohusiana na Hijja.

16. (1)Iwapo hujaji hakuweza kutekeleza ibada ya Hijja; au alitekeleza italazimu kutolewa gharama za ziada kwa sababu zilizo sababishwa na Kampuni; basi Kampuni hiyo italazimika kumpatia hujaji huyo nafasi ya kuhiji kama watakavyokubaliana na Kampuni bila ya Hajj kutakiwa kulipia gharama za ziada.

(2) Iwapo Hujaji hakuweza kutekeleza ibada ya Hijja au kukajitokeza gharama za ziada kutokana na sababu zilizotokana na Hujaji mwenyewe basi gharama hizo na matokeo yake yatabebwa na hujaji mwenyewe na iwapo atafariki basi yatatozwa katika tirka yake.

(3).Iwapo hujaji hakuweza kutekeleza ibada ya Hijja au kukajitokeza gharama za ziada kutokana na sababu zilizo nje Kampuni na Hujaji, Kampuni na Hujaji au warithi wake watazungumza namna ya kulisawazisha; sulhu isipofikiwa litafikishwa kwa Umoja, na sulhu isipofikiwa litafikishwa Kamisheni kwa kutolewa maamuzi.

Takaaful katika Hijja

17. (1) Kamisheni wanaweza kuweka Mfuko wa Takaaful ya Hijja ili kuwasaidia mahujaji, viongozi na wote wanaosimamia Hijja iwapo kutatokea janga lolote ikiwemo maradhi, ajali, na mfano wa hayo wakati wa maandalizi, safari au utekelezaji wa Hijja.

(2) Takaaful ya Hijja itaendeshwa kwa mujibu wa taratibu zitakazowekwa na

Kamisheni baada ya kushauriana na Umoja.

Uwezo wa Bodi katika kuweka miongozo

(3) Bila ya kuathiri masharti ya Kifungu 17 (1) na (2), fedha zinazobakia katika takaful ya Hijja kwa kila mwaka zitaingizwa katika Wakfu wa Hijja ambao utawekwa maalumu kwa kunufaisha shughuli za Hijja tu.

Makosa mbali mbali

18. Kwa kuzingatia Kifungu cha 55 (4) cha Sheria, Bodi inaweza kuweka Sharti, Utaratibu, Miongozo na kuidhinisha fomu za kiutendaji zitakazopelekea usimamizi mzuri wa shughuli za Hijja.

19. (1) Mtu yeyote ambaye:-

(a) atakwenda kinyume na matakwa ya Kanuni hizi;
(b) ataghushi, atapotesha au atatoa taarifa za uongo;
(c) atamchochea, atamshawishi mtu mwengine kufanya jambo lililokatazwa au kutokufanya jambo lililoamrishwa na Sheria au Kanuni hizi;

Atakuwa ni mkosa na akitiwa hatiani atapaswa kulipa faini au kifungo au vyote viwili kwa pamoja kwa mujibu wa kifungu cha Sheria

(2) Kiongozi yeyote wa Kampuni ambaye:-

(d) atakwenda kinyume na matakwa ya Kanuni hizi;
(e) ataghushi, atapotesha au atatoa taarifa za uongo;
(f) atamchochea, atamshawishi mtu mwengine kufanya jambo lililokatazwa au kutokufanya jambo lililoamrishwa na Sheria au Kanuni hizi;

Atakuwa ni mkosa na ikithibitishwa, Kamisheni inaweza kumzuwilia kujishughulisha na uongozi au usimamizi wa shughuli za Hijja kwa kipindi kisichopungua miaka mitano.

(4) Kiongozi aliyefukuzwa katika Kampuni au Umoja kwa:

a. Kutiwa hatiani kwa kufanya kosa la jinai;

b. Kuthibitika kufanya kosa la kinidhamu ambalo kwa mujibu wa maadili ya kiislamu linaondoa sifa ya uadilifu;

c. kutowajibika au kufanya jambo linaloweza kuharibu Hijja kwa mahujaji hatoruhusiwa kuongoza taasisi nyengine zenye Kibali ndani ya kipindi kisichopungua miaka kumi.

(5) Kampuni yoyote ambayo:-

a. Itakwenda kinyume na matakwa ya Kanuni hizi;

b. itaghushi, itapotesha au itatoa taarifa za uongo;

c. Itachochea, itamshawishi mtu au Kampuni kufanya jambo lililokatazwa au kutokufanya jambo lililoamrishwa;

itakuwa imekosa na ikithibitika inaweza kupewa onyo, kusimamishwa kwa muda au kufutiwa kibali cha kusafirisha mahujaji.

Marekebisho

20. Waziri kwa kutangaza kwenye Gazeti anaweza kurekebisha ama kubadilisha Kanuni yoyote iliyotajwa kwenye Kanuni hizi pindi akiona kuna haja ya kufanya hivyo.

IMETIWA saini leo tarehe...................mwezi wa..................................2019

..........................

KHAMIS JUMA MAALIM

Waziri wa Katiba na Sheria ZANZIBA